

# Milango ya utalii Ruvuma Imefunguka

Na Albano Midelo

## Masalia ya mijusi mitatu iliyoishi miaka milioni 240 yagundulika Ruvuma

MASALIO YA MIJUSI MITATU ILIYOISHI MIAKA MILIONI 240 YAGUNDULIKA PORI LA AKIBA LA LITUMBANDYOSI, BONDE LA RUHUU MKOANI RUVUMA



MASALIO ya aina tatu za mijusi ambayo inaaminika iliishi miaka milioni 240 iliyopita yamegundulika katika Pori la Akiba la Litumbandyosi, Bonde la Ruhuhu wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anasema ugunduzi huo licha kuongeza vivutio vya utalii katika Pori la Akiba la Litumbandyosi, lakini pia unaongeza vivutio vya utalii

katika Mkoa wa Ruvuma hali ambayo itafungua milango ya utalii.


Masalia ya mabaki ya mijusi hiyo, yamegundulika katika maeneo ya Manda, Lifua, Kingori na Usili ndani ya Bonde la Ruhuhu na kwamba masalia ya mijusi inaaminika imeishi miaka mingi zaidi duniani ukilinganisha na aina nyingine za masalia ya mijusi.

Tanzania imebahatika kuwa na masalia ya viumbe adimu duniani ambavyo vinavutia watalii kila kona hapa nchini kufika kufanya tafiti na kutembelea katika maeneo husika.

Moja ya vivutio hivyo ni masalia ya mijusi ambaye anafahamika kwa jina la Tendaguru anayepamba makumbusho ya Ujerumani ambaye masalia yake yaligundulika mkoani Lindi.

Masalia ya mijusi huyo yalivumbuliwa katika eneo la Tendaguru wilayani Kilwa mkoani Lindi zaidi ya miaka 100 iliyopita. Mjusi huyo ni kuvutio adimu katika Makumbusho ya Berlin nchini Ujerumani ambaye ana uzito wa tani 50.

Mjusi huyo kwa jina la kitaalam anaitwa dinosaurs ambapo masalia ya mijusi



huyo toka katika eneo la Tendaguru, yalikusanywa na kupelekwa Ujerumani ambako watalaam waliyaunda na kisha kuyaweka kwenye Makumbusho ya Berlin yali- ojengwa tangu mwaka 1889.

Mjusi huyo anakadiriwa kuwa na umri wa miaka milioni 150, ana urefu wa meta 13.7 kwenda juu, anakadiriwa kuwa na moyo wenye uzito wa kilo 400 na chakula cha mjusi huyo kilikuwa ni mimea.

Mwanasayansi na Mtafiti wa Mambo ya kale Dk. Daniela Schliart anasema mjusi huyo aligundulika kati ya mwaka 1907 na 1909 ambapo watafiti katika eneo la Tendaguru walikuwa wanatafiti madini ndipo walikutana na masalia hayo kisha kukusanya masalia na kuyasafirisha.

Ugunduzi wa masalia mengine ya mijusi katika Bonde la Ruhuhu mkoa wa Ruvuma yanafungua milango ya utalii katika ukanda wa kusini wenye mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara.

Wanasayansi waliogundua, aina tatu za masalia ya mijusi bonde la Ruhuhu wanazitaja aina hizo kuwa ni ruhuhuensis iliyo- gunduliwa katika eneo la Kingori, ruhuhuaria ambayo imegundulika eneo la Manda Lifua na masalia ya mijusi aina ya ruhuhucerberus eneo la

Kawinga.


Mgunduzi wa masalia ya mijusi ya ruhuhuaria anaitwa Fransis Perrington ambaye anaaminika aliyagundua kwa mara ya kwanza mwaka 1930 katika miamba tabaka ya Lifua Manda Bonde la Ruhuhu.

Masalia ya mjusi aina ya Ruhuhucerberus yaligundulika eneo la Kawinga mwaka 2002 na masalia ya awali ya mijusi ya ruhuhuensis iligundulika mwamba wa Usili Bonde la Ruhuhu mwaka 1950.

Hata hivyo Utafiti wa mwisho kuhusiana na masalia ya mijusi hiyo ulifanyika kati ya mwaka 2007 na 2008 na Timu ya watafiti toka nchi za Uingereza na Marekani na ku- gundua idadi kubwa ya masalia ya mijusi hiyo katika Bonde la Ruhuhu.

Watafiti hao wa kima- taifa wa Ma- kumbusho, wakioongoz wa na Ken Angielzyk na Bill Simpson walikuwa ni miongoni mwa wanasayansi wa kimataifa waliofika Bonde la Ruhuhu kufanya uchunguzi na kufanikiwa kukusanya idadi kubwa ya ma- salia ya mijusi ambayo inaaminika iliishi mi- aka mingi zaidi duni- ani.

“Masalia haya ya mijusi jamii ya mamba yalijadiliwa katika nyaraka (Thesis) kadhaa katika chuo kikuu cha Cam- bridge, Uingereza, inaka dirwa kwamba jamii hiyo ya mijusi iliishi bonde la Ruhuhu mi- aka milioni 240 iliyo- pita”, anasema Afri- kanus Challe Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma.



Kulingana na vipimo vya kiikolojia kwenye mabaki ya mijusi hiyo, inaaminika dinosaurs wa Bonde la Ruhuhu ana urefu wa meta kati ya 2.7 hadi 10, ana shingo ndefu na mkia, na alikuwa na miguu minne kama mamba.

Challe anasema ugunduzi wa masalia ya mijusi katika bonde la Ruhuhu ni mafanikio makubwa kwa wanasayansi hao kwa sababu wamegundua kile wanachoita kama ni chanzo cha kizazi cha dinosaurs na kwamba ugunduzi huo mpya umejaza pengo kubwa katika historia ya mabaki ya mijusi huyo adimu duniani.

Kwa mujibu wa wagunduzi wa mabaki ya mijusi hiyo, ugunduzi huo unaaminika kuwa ni wa dinosaurs mwenye umri mkubwa kuliko wote duniani na rekodi za mabaki zinaonesha kwamba zilikuwapo baada ya kikundi kikubwa cha viumbe vilivyoitwa archosaurs, ambavyo viliwekwa katika makundi mawili ya ndege na mamba.

Uchunguzi umebaini kuwa miaka ya 2007 hadi 2008 watafiti hao wa kimataifa wa mambo ya kale, walirudi tena katika Bonde la Ruhuhu, ili kuangalia sehemu za mabaki ya mijusi hiyo ambazo zilipotea na kufanikiwa kupata mabaki ambayo yalikuwa na uhusiano na mabaki ya dinosaur kwa kwanza.

Wataalam hao wakiongoza na Rex Parrington walipata mabaki ya mijusi akiwa na mkia wenye mrefu wa mita 1.5, uzito wa kilogram 60 ambapo asilimia zaidi ya 90 ya mijusi hao imetoweka duniani.

Timu ya wanasayansi kutoka Makumbusho ya Historia ya London nchini Uingereza na Chuo Kikuu cha California na Chuo Kikuu cha Washington nchini Marekani wanaeleza kuwa mabaki ya mijusi wa bonde la Ruhuhu yanaweza kuwakilisha dinosaur wa kale zaidi ambaye aliishi Tanzania zaidi ya miaka milioni 240 iliyopita.

Ugunduzi wa masalia ya mijusi hiyo upo ndani ya Pori la Akiba la Litumbandyosi mkoani Ruvuma. Mchakato wa kuhifadhi eneo la Litumbandyosi kuwa Pori la wanyamapori ulianza tangu mwaka 2003 kwa Idara ya Wanyamapori kuendesha mikutano ya awali na serikali za vijiji vinavyozunguka katika eneo hilo vikwemo vijiji vya Litumbandyosi, Kingore, Paradiso, Luhagara, Ruan da, Mtunduwalo na Ndongosi.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anasema Pori la Akiba la Litumbandyosi lenye ukubwa wa kilometa za mraba 494 ni moja kati ya mapori ya akiba matatu yaliopo mkoani Ruvuma.

Mapori mengine anayataja kuwa ni Liparamba na Gesimasowa ambayo ni mapito ya wanyamapori kutoka Pori la Akiba la Selous hadi katika hifadhi ya Niassa iliyopo nchini Msumbiji hivyo ni vema maeneo hayo kuhifadhiwa na kulindwa.

Challe anasisitiza kuwa mkoa wa Ruvuma unaboresha mapori ya Akiba ili kuungana na serikali katika lengo lake la kuendeleza utalii katika kanda ya kusini ambao bado haujapewa kipaumbele kama ilivyo katika mikoa mingine.

Anasema wananchi wa mikoa ya kusini ukiwemo mkoa wa Ruvuma bado hawajanufaika katika sekta ya utalii moja ya sababu kubwa ni kwamba wananchi wa mikoa ya kusini hawajapata elimu ya kutosha kuhusu faida za utalii.

“

## Utalii Kusini

“ili kuongeza wigo katika sekta ya utalii, Halimashauri ya wilaya Mbinga imependekeza kutenga pori la akiba la Litumbandyosi kwa ajili ya hifadhi ya wanyama pori baada ya kuwashirikisha wananchi wanaozunguka vijiji vya hifadhi hiyo”, anasisitiza Challe.

Kamanda wa kikosi cha kuzuia ujangili kanda ya kusini Msonda Simwanza anasema utalii sio kuona wanyamapori pekee bali ni pamoja na shughuli za kiasili na kipekee zinazofanywa katika maeneo yao na kuweka mazingira ya utalii endelevu kama ugunduzi wa masalia ya mijusi adimu duniani.

Simwanza amewapongeza wananchi wanaozunguka pori la Litumbandyosi kwa kuridhia kuwepo kwa pori hilo ambalo amesema litawawezesha wananchi hao kupata maendeleo makubwa baada ya wawekezaji kufika kuwekeza.

“Utalii ni pamoja na kusafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, kufanya utafiti na kuona shughuli zinazofanywa na watu katika maeneo husika, sio kuangalia wanyamapori pekee”, anasema.

Kulingana na Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma, Pori la Litumbandyosi linafaa kuwa hifadhi ya wanyama kwa kuwa lina wanyama na ndege wa aina mbalimbali kwa kuwa lipo katika mfumo wa Pori la Akiba la Selous (Selous Eco System).

Anawataja wanyama waliopo katika pori hilo ambao wanatoka katika Pori la Akiba la Selous kuwa ni kiboko, nyati, parahala, nyani, nguruwepori, chui, pofu, swala, tembo, faru na aina mbalimbali za ndege wakiwemo kware, kanga na njiwa.

“Eneo hili lipo katika ukanda wa uhamiaji wa wanyama kutoka hifadhi ya wanyama ya Selous ambako kuna wanyama wengi, wanyama hao wamekuwa wakiingia katika pori la Litumbandyosi kupitia ushoroba uliopo katika maeneo ya Lutukira, Hanga Gumbiro na Ngadinda wilayani Songea”, anasisitiza.

Anayataja madhumuni makubwa ya serikali katika sekta ya utalii hivi sasa kuwa ni kujaribu kupanua wigo wa utalii kusini mwa Tanzania kwa kutambua vivutio vya utalii vilivyopo kusini na kuviuza nje ya nchi ili wananchi waweze kunufaika navyo.

“Tunatekeleza maagizo ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha vivutio vya utalii vilivyopo kanda ya kusini vinaibuliwa na kutangazwa, vivutio vyetu sisi ni tofauti na vya ukanda wa kaskazini ambayo vingi ni hifadhi za wanyamapori, watalii wanaoingia nchini hivi sasa itabidi waje kusini kuona vivutio ambavyo havipatikani sehemuningine yoyote duniani”, anasisitiza Challe..



Mwandishi wa makala haya ni  
Albano Midelo ambaye ni Afisa Habari  
Mkoa wa Ruvuma  
Mawasiliani yake ni  
Barua pepe [albano.midelo@gmail.com](mailto:albano.midelo@gmail.com)  
Simu 0784765917